

Meza ya Bwana

“Meza ya Bwana ni kushiriki katika mfano wa mwili na damu ya Yesu kama udhihirisho wa imani katika Yeye, Bwana na Mwokozi wetu. Katika uzoefu huu wa ushirika, Kristo anakuwepo kukutana na kuwaimarisha watu wake. Tunapotwaa (mkate na divai) kwa furaha tunatangaza mauti ya Bwana hata arudipo tena. Maandalizi ya Meza ya Bwana hujumuisha kujihoji nafsi, toba na ungamo. Bwana aliagiza huduma ya kutawadhana miguu ili kukumbusha utakaso mpya, kuonyesha nia ya kutumikiana sisi kwa sisi katika unyenyekevu unaofanana na wa Kristo, na kuungana mioyo yetu katika upendo. Huduma ya Meza ya Bwana ni ruhusa kwa waumini wote Wakristo. (1Kor.10:16, 17; 11:23-30; Mt.26:17-30; Ufu.3:20; Yoh.6:48-63; 13:1-17).

Wakiwa na miguu iliyojaa vumbi, waliingia kwenye chumba cha juu kwa ajili ya Pasaka. Moja alikuwa ameandaa mtungi wa maji, bakuli na kitambaa kwa ajili ya desturi ya kutawadha miguu, lakini hapakuwepo aliyekuwa tayari kufanya kazi dhalili. Akitambua juu ya mauti yake inayomsogelea, Yesu alisema kwa huzuni “nimetamani sana kula pasaka hii pamoja nanyi ... kwa maana nawaaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. (Luk.22:15, 16). Kuoneana wivu miongoni mwa wanafunzi kulimtia Yesu huzuni. Bado walikuwa wakishindana nani ni mkubwa kwenye ufalme wa Mungu. (Luk.22:24; Mt.18:1; 20:21). Je, wangeweza kujifunza kuwa kwenye ufalme wa Mungu ni kutumika kwa unyenyekevu?

“Hata wakati wa chakula cha jioni” (Yoh.13:2, 4), Yesu kimya kimya aliinuka, akachukua kitambaa, akamimina maji kwenye bakuli, akapiga magoti na akaanza kuwatawadha wanafunzi wake. Hata alipomaliza, alirejea kwenye sehemu yake akawaambia “Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea? Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Amini amin, nawaaambia ninyi Mtumwa si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda” Yoh. 13:12, 14, 16-17).

Hivyo ndivyo Yesu alivyoanzisha malali pa Pasaka, huduma ambayo ingetambulisha kafara yake kuu, Meza ya Bwana. Aliuchukua “mkate usiotiwa chachu, akaubariki na kuuvunja na kuwapa wanafunzi wake akawaambia twaeni mle huu ni mwili wangu ambao umevunjwa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa kumbukumbu yangu”. Kisha akachukua kikombe cha Baraka “akashukuru na kuwaambia nyweeni wote katika hiki . Kwa kuwa hii ni damu yangu ya agano jipya iliyomwagika kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu.” Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. (Angalia Mt.26:26-28; 1Kor.11:24-26; 10:16). Kwa jinsi hii alianzisha desturi hizi ili tuwe na ushirika naye.

Agizo la Kuoshana Miguu

Desturi ilihitaji katika kusherehekea Pasaka, familia za Kiyahudi kuondoa chachu yote, ikimaanisha dhambi, kutoka kwenye nyumba zao kabla ya siku ya kwanza ya mikate (Kut.12:15, 19, 20). Kwa hiyo waumini wapaswa kuungama na kutubu dhambi zao pamoja na kiburi, ushindani, wivu, hisia za hasira na ubinafsi, kabla ya kuwa na ushirika na Yesu.

Yesu alianzisha desturi ya kuoshana miguu na kuagiza wanafunzi wake nao watende hivyo hivyo, “mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda” (Yoh.13:17). Agizo hili linalotangulia Meza ya Bwana hutimiza kule kujihoji mtu mwenyewe kwanza ili kutokushiriki kwa namna isiyostahili. (1Kor.11:27-29).

Maana ya Agizo. Kuoshana miguu hudhihirisha jambo muhimu kuhusu utume wa Kristo na uzoefu wa mshiriki.

1. Ukumbusho wa kujishusha kwa Kristo. Kuoshana miguu hukumbusha unyenyekevu wa Kristo katika kufanyika kwake mwili. Akiwa na hadhi ya juu mbinguni alishuka chini akawa namna ya mtumwa (Wafil.2:7). Ilikuwa kujishusha kwa Mwana wa Mungu kwa kutoa pasipo ubinafsi na kuishia kukataliwa na kusulubiwa kama mkosaji! Kristo alikuja kutumika siyo kutumikiwa (Mt.20:28). Kwa kuwaosha wanafunzi miguu alionyesha huduma ya unyenyekevu. Kwa kumfuata, twapaswa kutumikiana kwa upendo. (Gal.5:13). Huduma hii haidhalilishi kwa kuwa kwa kusohana miguu, huwa kielelezo kuwa tunamwosha miguu Kristo. “Kadiri tunavyomtendea mojawapo, huwa tunamtendea Kristo.” (Mt.25:40).

2. Mfano wa Kutakaswa. Kuosha miguu kulifanya makubwa zaidi ya kusafisha miguu – ilisafisha moyo. Petro alipoomba aoshwe mwili mzima, Yesu alisema haina haja kwani tayari ni safi isipokuwa miguu. (Yoh.13:10). Kama wafuasi wa Kristo, tulikwisha batizwa lakini mwenendo wetu hufanya tuchafuke miguu na hivyo hitaji la kuosha. Hivyo huduma hii hutukumbusha hitaji letu la kuendelea kutegemea damu ya Kristo kwa utakaso.

3. Ushirika wa Kusameheana. Mtazamo wa kusameheana miongoni mwa wanaoshiriki huduma hii humaanisha kusudi lake la kuongoza kusameheana limetimizwa. Ni pale tu tunaposamehe wengine ndipo nasi tunasamehewa na Baba yetu aliye mbinguni. (Mt.6:14, 15).

4. Ushirikiano pamoja na Kristo na waumini. Kuosha miguu hudhihirisha Kristo alivyowapenda wafuasi, kwa upeo. (Yoh.13:1). Petro aliposita na kusema “huwezi kunitawadha miguu kamwe”, Yesu alijibu “kama nisipokutawadha, huna shirika nami” (Yoh.13:8). Jioni hiyo hiyo, Yesu alitoa amri mpya ya kupendana (Yoh.13:34). Ujumbe wa agizo uko wazi, kuwa tumikianeni kwa upendo. (Gal.5:13). Kwa kutumikia wengine, maana yake tunawahesabu wengine kuwa bora kuliko sisi (Wafil.2:3). Pia hutubidisha kuwajali na kuwapenda hata wale wanaotofautiana nasi.

Kusherehekea Meza ya Bwana

Miongoni mwa majina maarufu yanayotumiwa na Waprotestanti kwa ajili ya huduma ya ushirika, ni chakula cha Bwana (1Kor.11:20). Mengine ni Meza ya Bwana (1Kor.10:21), kumega mkate (Mdo.20:7; 2:42) na Ekaristi ikihusisha kushukuru na baraka vinavyofanyika wakati wa huduma hiyo (Mt.26:26, 27; 1Kor.10:16; 11:24). Meza ya Bwana ni wakati wa furaha siyo wa huzuni. Baada ya kuoshana miguu, kujihoji, kuungama dhambi, kusuluhisha tofauti na msamaha, kupokea uhakika wa kusafishwa na damu ya Yesu, huwa tunageukia meza tayari kuingia kwenye ushirika na Bwana.

Maana ya Chakula cha Bwana. Meza ya Bwana imechukua nafasi ya sherehe za Pasaka za kipindi cha Agano la Kale. Pasaka ilitimizwa Kristo, mwanakondoo wa Pasaka alipoutoa uhai wake. Kristo mwenyewe alianza Meza ya Bwana, sherehe kubwa ya Waisraeli wa kiroho. Hivyo mizizi ya kielelezo cha Meza ya Bwana inavuka hadi nyuma hadi kwenye sikukuu ya Pasaka.

1. Kukumbuka kuokolewa kutoka dhambini. Kama ambavyo Pasaka ilikumbusha Waisraeli walivyokombolewa kutoka utumwani Misri, Meza ya Bwana inatukumbusha tulivyokombolewa kutoka kwenye Misri ya kiroho, kutoka kwenye utumwa wa dhambi. Damu ya mwana kondoo ilipakwa kwenye vizingiti na miimo ya milango na nyama yake iliwapa nguvu Waisraeli kuondoka Misri (Kut.12:3-8). Kafara ya Kristo huokoa kutoka mauti na waumini wanaokolewa kwa kula mwili na kunywa damu ya Yesu. (Yoh.6:54). Vivyo hivyo Meza

ya Bwana hutangaza kwamba mauti ya Kristo msalabani ilifanya wokovu wetu, ikitoa msamaha na amana (garantii) ya uzima wa milele.

Yesu alisema “fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu (1Kor.11:24). Agizo hili husisitiza kule kuchukua nafasi ya jambo jingine ambako kafara ya Yesu ilitimiza. “Huu ni mwili wangu” Yesu akasema “ulio kwa ajili yenu” (1Kor.11:24 cf. Isa.53:4-12). Msalabani, asiye na hatia alichukua sehemu ya mwenye hatia, mwenye haki akachukua sehemu ya wasio haki. Jambo hili lilitimiza madai ya sheria kwa kifo cha mwenye dhambi, kikileta msamaha, amani, uhakika wa uzima wa milele kwa mwenye dhambi atubuye. Msalaba uliondoa hukumu na kutuvika vazi la haki ya Kristo na uwezo wa kushinda dhambi.

a. Mkate na tunda la mzabibu. Yesu alitumia vielelezo vingi kufundisha kweli mbalimbali kumhusu. Mimi ndimi mlango (Yoh.10:7), Mimi ndimi njia (Yoh.14:6), Mimi ndimi mzabibu wa kweli (Yoh.15:1), mimi ndimi chakula cha uzima (Yoh.6:35). Hatuwezi kutumia maelezo haya kama yalivyo kwa kuwa hayupo katika kila mlango, njia au mzabibu. Badala yake vina maana ya ndani zaidi. Alipolisha watu 5,000, Yesu alidhihirisha umuhimu wa kina wa mwili na damu yake. Yesu alisema “siye Musa aliyewapa chakula kile cha mbinguni bali Baba yangu anawapa ninyi chakula cha kweli kitokacho mbinguni. Kwa maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinuni na kuupa ulimwengu uzima”. Wakamwambia “utupe chakula hiki”, Yesu akajibu “Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe” (Yoh.6:32-35). Alitoa mwili wake na damu yake kuzima njaa na kiu ya mahitaji yetu na matamanio yetu (Yoh.6:50-54).

Mkate wa Pasaka ambao Yesu alikula ulikuwa haujaumuliwa na tunda la mzabibu ambalo halijachachushwa. Chachu inayofanya mkate uumuke ilikuwa alama ya dhambi (1Kor.5:7, 8) na kwa hiyo isingefaa kuwa kielelezo cha mwanakondoo asiye na ila (1Pet.1:19). Vile vile ni mkate usioumuliwa na tunda la mzabibu lisilochachushwa ndivyo kwa usahihi, hufanya ishara ya damu itakasayo ya Kristo, isiyo na doa wala waa.

b. Kula na kunywa. “Msipoula mwili wake mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.” (Yoh.5:53, 54). Kula mwili wa Kristo na kuinywa damu yake ni lugha ya ishara ya kuliadini Neno lake, kwa namna ambayo huwafanya waumini waendeleo kuwasiliana na mbingu na kuwafanya wapate uzima wa kiroho. Asema “maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.”(Yoh.6:63). “Mtu hataishi kwa kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” (Mt.4:4).

Waumini humla Kristo, mkate wa uzima kupitia Neno la uzima, Biblia. Kwa hilo tunapata uwezo wa Kristo.

Katika huduma ya mkate tunabariki kikombe (1Kor.10:16). Hii humaanisha kama Kristo alishukuru kwa ajili ya kikombe (Mt.26:27), ndivyo nasi tunatoa shukrani kwa damu ya Yesu.

2. Kushiriki mwili wa Kristo. Katika ulimwengu uliojaa vurugu na mgawanyiko, kushiriki kwetu sherehe ya Meza ya Bwana huchangia umoja na uimara wa kanisa, tukionyesha kuwa tu washirika na Kristo na washiriki sisi kwa sisi. (1Kor.10:16, 17). Kuzembea katika huduma hii kunaleta hasara na inatimiza unabii “siyo wote ni wasafi”. Wakati katika jamii kuna kila kinachotufanya tutengane, tunatambua katika Kristo, tuna kila kinachotufanya tuungane. “Nyweeni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. (Mt.26:27, 28; Luk. 22:20). Jinsi ambavyo agano la kale lilithibitishwa kwa damu (Kut.24:8), agano jipya linathibitishwa na damu ya Kristo. Katika agizo hili, waumini hufanya upya ahadi zao kwa kuendelea kumtii na kumwamini Bwana na mwokozi wao.

3. Kutarajia ujio wa Bwana mara ya pili. “Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.” (1Kor.11:26). Huduma ya Meza ya Bwana inafanyika katikati ya siku ya Kalvari na siku ambayo Yesu atarudi tena na kuunganisha msalaba na ufalme wa utukufu. Kiapo cha Kristo “Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu” (Mt.26:29) ni unabii. Inaashiria karamu tutakayokula pamoja na mwokozi katika ufalme wa milele. Sherehe itakuwa kubwa maana ni arusi ya mwanakondoo (Ufu.19:9). Katika kujiandaa kwa siku hiyo, Kristo aliasa, “Viuno vyenu viwe vimefungwa, na taa zenu ziwe zinawaka, nanyi iweni kama watu wanaomngojea bwana wao atakaporudi kutoka arusini ili atakapokuja na kubisha, wamfungulie mara. Heri watumwa wale ambao bwana wao ajapo atawakuta wanakesha. Amin nawaambieni, atajifunga na kuwakaribisha chakulani, atakuja na kuwahudumia. (Luk.12:35-37).

Sifa za kushiriki Meza ya Bwana.

Desturi mbili hutumika kwa imani ya Kikristo, Ubatizo na Meza ya Bwana. Yesu aliendesha huduma ya Meza ya Bwana kwa wafuasi wake tu, hivyo huduma hii ni kwa wakristo waaminio tu. Biblia hualika waumini kula kwa namna inavyostahili (1Kor.11:27). Mara nyingine isivyostahili ni huhusu utaratibu wa kupokea mkate na kula kabla ya wengine (1Kor.11:21) au kwa kukosa imani itendayo kazi katika Kristo. Kutenda isivyostahili katika jambo hili ni kujipatia hukumu. (1Kor.11:29). Inashauriwa kabla ya kula na kunywa katika Meza ya Bwana, kujihoji, kwa maombi unajipima moyoni mwako na kuungama dhambi na kurejesha mahusiano yaliyovurugika. Kujihoji ni jambo la mkristo binafsi. Ni kweli dhambi za wazi huzuia muumini asishiriki Meza ya Bwana (1Kor.5:11), ikikumbukwa kuwa Yesu alikubali kula pamoja na Yuda aliyekuwa kwa nje ni mfuasi wake kumbe moyoni ni mwizi. Kinachozingatiwa ni hali ya moyo. Wote wanakaribishwa kushiriki katika huduma hii.